OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA HANANG'
SHULE YA SEKONDARI MASAKTA
S.L.P 231, KATESH. SIMU: 0784 857 670 / 0767 888 125

21/12/2020

HANDC NA/MSS/J.1/12

MWANAFUNZI .....

SHULE YA MSINGI .....

S.L.P .....

YAH. KUCHAGULIWA KWAKO KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MASAKTA KIDATO CHA KWANZA 2021

Ninayo furaha kukujulisha rasmi kuwa wewe ni mojawapo kati ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na shule hii.

Nachukua nafasi hii kukupongeza kwa kupata nafasi hii ambayo wengi wanaitamani lakini wameshindwa kuipata. Kupatiwa nafasi hii ni bahati tu, hivyo ni matumaini yangu kuwa utafanya kila lililo katika uwezo wako ili nafasi uliyoipata itumike hasa kusoma kwa bidii, maarifa na nidhamu.

Unatakiwa kuripoti tarehe **11/01/2021** saa **01:00 asubuhi.** Hivyo ufikapo shuleni wasiliana na Makamu Mkuu wa shule ukiwa na fomu ya uthibitisho wa daktari, fomu ya kukubali nafasi ya shule na mahitaji mengine yote yaliyoorozeshwa.

Mwanafunzi atakayechelewa zaidi ya wiki moja baada ya tarehe ya kufungua shule atahesabiwa kuwa ni mtoro na atachukuliwa hatua za kisheria. Aidha nasisitiza kwamba ni vema kila mwanafunzi akahudhurie shule katika juma la kwanza kwa sababu atapata fursa nzuri ya kuelimishwa na kuelekezwa masuala mbalimbali ya taaluma, nidhamu, malezi, sheria za shule, n.k.

Karibu sana.

_____

Mkuu wa Shule

MAHITAJI YA MWANAFUNZI

1. SARE ZA SHULE 2021

1.1 WAVULANA

(i) Suruali rangi ya kijivu (celebration).
(ii) Shati nyeupe mikono mifupi (tetron).
(iii) Soksi rangi ya kaki ndefu.
(iv) Sweta rangi ya kijivu.
(v) Viatu vyeusi vya kamba, kisigino kifupi.
(vi) Ufagio mmoja kwa ajili ya matumizi ya mwanafunzi.
(vii) Nguo za michezo; tracksuit (kijivu) na raba za michezo.
(viii) Ndoo moja.

1.2 WASICHANA

(i) Sketi rangi kijivu aina ya rinda box (ndefu inayovuka magoti)
(ii) Shati / blauzi nyeupe mikono mifupi (tetron).
(iii) Soksi rangi nyeupe, ndefu.
(iv) Sweta rangi ya kijivu.
(v) Viatu vyeusi vya kamba, kisigino kifupi.
(vi) Ufagio mmoja kwa ajili ya matumizi ya mwanafunzi.
(vii) Nguo za michezo; tracksuit (kijivu) na raba za michezo.
(viii) Ndoo moja.

2 MAHITAJI YA CHAKULA

(i) Mahindi debe nne (4) kwa mwaka.
(ii) Maharage galoni sita (6) kwa mwaka.
(iii) Fedha tasilimu Tshs 60,000/= (sitini elfu tu) kwa mwaka.

Zingatia:

(a) Wanafunzi wote lazima wapate chakula cha mchana shuleni kwa maendeleo yao kitaaluma na afya zao. Vinginevyo utawajibika kwa kutomtunza mtoto wako.
(b) Unaruhusiwa kulipa kwa awamu mbili; Januari 2021 na Julai 2021
(c) Fedha zote taslimu ziwekwe katika akaunti ya chakula iliyoko benki ya NMB. Jina la Akaunti ni KAMATI YA CHAKULA MASAKTA SEC. SCHOOL, Namba ya Akaunti ni 41010006859. Kumbuka kuleta karatasi ya kuwekea fedha (Pay in Slip) shuleni kwa ajili ya kumbukumbu.

3 MENGINEYO

(i) Kila mwanafunzi aje na vifaa vya kujifunzia ambavyo ni; four figure table, kamusi / dictionary, graph paper, rula, na mkebe (mathematical set).
(ii) Kila mwanafunzi aje na daftari kumi na mbili (12) aina ya counter book zenye 3 quire kwa ajili ya masomo.
(iii) Kila mwanafunzi aje na karatasi (Ream Paper, A4), Bunda moja.
(iv) Kila mwanafunzi aje na jembe moja, lenye mpini wake.

SHERIA ZA SHULE

A. HESHIMA

(i) Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na heshima kwa walimu, wafanyakazi wote wa shule, wao kwa wao na mtu mwingine yeyote.

(ii) Wanafunzi hawaruhusiwi kutumia lugha yeyote mbaya wakati wowote kati yao wenyewe, kwa walimu wao na kwa watu wengine

(iii) Wanafunzi wote ni lazima washirikiane na kusaidiana na waheshimu na kuthamini kazi za aina zote.

(iv) Wanafunzi wote hawaruhusiwi kufanya mambo yafuatayo:-

(a) Kuvuta sigara au bangi na kutumia madawa ya kulevya.

(b) Kunywa pombe.

(c) Kuvaa mavazi yasiyo ya heshima.

(v) Wanafunzi wanatakiwa kuitikia mara kwa mara na kukimbia wanakoitwa.

(vi) Wanafunzi wanatakiwa kuheshimu bendera ya serikali, picha za viongozi wa serikali, Wimbo wa Taifa na fedha za Taifa.

(vii) Wanafunzi waheshimu ukumbi wa mikutano, ofisi za shule, kutunza na kuthamini mali ya binafsi na mali ya umma.

(viii) Wanafunzi wote wawe mfano mzuri wa heshima na tabia njema mahali popote walipo.

(ix) Wanafunzi hawaruhusiwi kupiga kelele wakati wote akiwa darasani, wasitoke nje bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi aliyeko.

(x) Wanafunzi wanyoshe mikono juu na wasimame wanapoulizwa na kujibu maswali.

(xi) Uhusiano kati ya wavulana na wasichana uwe wa kimasomo tu.

(xii) Wanafunzi hawaruhusiwi kuwa na simu na ikibainika ATAFUKUZWA SHULE.

B. MAHUSIANO

(i) Ni lazima wanafunzi wote wahudhurie vipindi vyote ndani na nje ya darasa.

(ii) Wanafunzi wote ni lazima wahudhurie kazi zote za mikono

(iii) Wanafunzi wote ni lazima wahudhurie mikutano ya shule ikiwemo; baraza la shule, ukaguzi wa usafi, kupandisha Bendera ya Taifa, n.k.

(iv) Kwa kuzingatia sheria ndogo ya mahudhurio ya lazima katika shule za sekondari Wilaya ya Hanang' **mwanafunzi atakayekosa / acha shule bila sababu ya msingi, pamoja na mzazi / mlezi atakayesababisha mwanafunzi kuacha shule / masomo atachukuliwa hatua za kisheria** kwa kuzingatia sheria ndogo hiyo

C. KUWAHI

(i) Wanafunzi wote ni lazima wawahi katika shughuli zote za shule kama zilivyo pangwa katika ratiba ya kila siku, kama vile vipindi vya darasani na nje ya darasa, wakati wa zamu, kurudi shule baada ya likizo, n.k.

(ii) Wanafunzi ni lazima wawahi haraka wanaposikia wito wa dharula.

FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA SHULE NA MASHARTI YAKE

MKUU WA SHULE,
SHULE YA SEKONDARI MASAKTA,
S.L.P 231,
KATESH – HANANG'
MANYARA.

A. MWANAFUNZI

Mimi _____ nimesoma kwa makini barua ya maagizo ya kujiunga na shule ya sekondari Masakta, pamoja na sheria zake.

Kwa heshima na unyenyekevu na mkubwa naikubali* / ninaikataa nafasi hiyo kwa sababu _____

Pia nayakubali* / nayakataa masharti na sheria za shule ya sekondari Masakta.

_____ ___ / ___ / 20___
Saini ya Mwanafunzi Tarehe

B. MZAZI / MLEZI

Mimi _____ mzazi / mlezi wa mwananafunzi _____ ambaye amechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Masakta nimesoma maagizo ya kujiunga na sheria za shule. Ninakubali / ninakataa nafasi hiyo, ninaahidi* / siahidi kumtimizia mtoto wangu mahitaji na maagizo yote ya kujiunga na shule kwa muda uliopangwa.

Aidha naahidi* / siahidi kushirikiana daima na uongozi wa shule katika kumkuza na kumlea mtoto huyu kwa manufaa yake binafsi, wazazi na Taifa kwa ujumla.

Kama unakataa, sababu ya kukataa _____
_____
_____

Zingatia:
Udanganyifu wowote ambao utasababisha / lenga kumkosesha mwanafunzi masomo / shule hautavumiliwa

Jina na Anuani ya Mzazi / Mlezi: _____
_____ Saini ya Mzazi / Mlezi
_____ ___ / ___ / 20___
_____ Tarehe

(Kata neno lisilohusika)

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA HANANG'
SHULE YA SEKONDARI MASAKTA
S.L.P 231, KATESH. SIMU: 0784 857 670 / 0767 888 125

MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by Government Medical Officer

Pupil full name: _____

Age: _____

Blood count (Red and White): _____

Stool Examination: _____

Urinalysis: _____

Syphilis Test: _____

T.B Test: _____

Eye Test: _____

Ears: _____

Chest: _____

Spleen: _____

Abdomen: _____

Additional information: E.g. Physics defects or impairment, infection, chronic of family diseases, etc.

_____

_____

_____

_____

CERTIFICATION OF GOVERNMENT MEDICAL OFFICER

I certify that the above mentioned pupil is fit to pursue his / her secondary school education.

Signature: _____ Designation: _____

Station: _____ Date: _____